Adamu wa Kwanza na Adamu wa Pili

(The First and Second Adam)

Na

Ellis P. Forsman

Adamu wa Kwanza na Adamu wa Pili

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Adamu wa Kwanza na Adamu wa Pili

1 Kor. 15:45-49

1 Kor. 15:45-49, "*Ndivyo ilivyoandikwa, mtu wa kwanza Adamu akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa mwisho ni roho yenye kuhuisha. Lakini hautangulii ule war oho, bali ule wa asili; baadaye huja ule wa roho. Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni. Kama alivyo yeye wa udongo, ndivyo walivyo wa udongo; na kama alivyo yeye wa mbinguni, ndivyo walivyo walio wa mbinguni. Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhaalika tutaichukua sura yake yeye aaliye wa mbinguni.*"

Kifungu hiki kinaonyesha Adamu wawili.

Mtume aliyevuviwa anaonyesha ameonyesha katika msitari wa 44, "*... kuna mwili asili, na mwili wa kiroho.*"

Sasa anaelezea hili kwa ulinganifu wa Adamu wawili.

Katika msitari 45 anaonyesha kwamba tukiwa na mwili wa asili, mwili wa mnyama tuliona kutoka kwa Adamu ulimwenguni hapa, pia tunawezaa kutarajia mwili wa kiroho kutoka kwa Kristo, Adamu wa pili.

Hivyo basi, kama tupo ndani ya Kristo, inawezekana kwamba tutakuwa na miili ya kiroho, kama ilivyo kwamba tuna miili ya asili au ya wanyama.

Hivyo, wafu wafao katika Kristo siyo tu kwamba watafufuliwa tu, bali zitafufuliwa zikiwa zimebadilishwa. Unaoharibika ulitokana na Adamu, bali usioharibika ulitoka kwa Yesu Kristo.

Kama uzao wa Adamu, sote tumezaliwa kwa muonekano na utii katika aina ya majaribu: dhambi, kifo, na uharibifu.

Lakini tukiwa wake Kristo, tutafufuliwa kubeba sura yake na kufurahia maisha ya kutoharibika kama yale anayofurahia sasa.

- Kol. 3:4, "*Kristo atakapofufuliwa aaliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafufuliwa pamoja naye kaatika utukufu*."
- 1 Yohana 3:2, "*Wapenzi sasa tu wana wa Mungu, wala haijarihirika bado tukavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.*"

Kuhusu Adamu, Paulo alisema katika Rom. 5:14, kwa yeye ni "*...Walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata hao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, aliyemfano wake yeye atakayekuja.*"

Tutaangalia yafuatayo:

- Ulinganifu kati yao – kufanana kwao.
- Tofauti kati yao – kutokufanana kwao.

Ulinganifu kati ya Adamu wawili

Mungu aliwaweka wote wawili duniani kwa miujiza.

Uwepo wa kila mmoja haukuwa kulingana na sababu ya kawaida ya asili.

Hakuna kilichotokana na sheria ya kawaida ya kizazi.

Wa kwanza alitengenezwa kutokana mavumbi ya ardhi, na wa pili mimba ilitungwa na Roho Mtakatifu.

Ebu tuangalie:

Uumbaji wa Adaamu.

Mwa. 2:7, "*BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.*"

Huu ulikuwa ni muujiza – kutolewa katika sheria ya asili. Hatuelewa uwezo wa Mungu.

Lakini tunaikubali kwa imani; hatuwezi kuielezea isipokuwa kwa imani.

Kuzaliwa kwa Yesu.

Kwamba Mungu akamweka Adamu wa pili juu ya ulimwengu kwa muujiza pia ni swala la imani. Hatuwezi kuielewa, isipokuwa imani.

Muungu aliyeufanya ulimwengu, na akawafanya watu wawili, na akawapa uwezo wa kuzaa, akaweka uwezo katika tumbo la bikira Mariamu.

Waandishi wawili wa injili wanatupatia idadi yake. (Mat. 1:18-23 na Luka 1:26-38).

Kila Adamu alikuwa na asili yenye uwezo wa kujaribiwa.

Majaribu ni sifa ya kila kilichoumbwa.

Ambapo hakuna uwezo wa kufanya ubaya hakuna wema katika kutunza haki.

Adamu wa kwanza alijaribiwa na akashindwa; Adamu wa pili alijaribiwa, lakini akashindwa.

- Mat. 4:1-11, "*Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamuijia akamwambia, ikiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akaajibu akasema imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kisha ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, atakuagiziaa malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, tena imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu wako. Kisha ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu na fahari yake, akamwambia haya yote nitakupa ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, nenda zako shetani; kwa maana imeandikwa msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. Kisha ibili akamwa; na tazama, wakaja malaika wakamtumukia.*"
- Heb. 4:15, "*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*"

Mungu aliwapa majina wote.

Mungu alimwita Adamu. Mwa. 5:2, "*Mwanaume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.*"

Mungu alimwita Yesu.

Fil. 2:9, "*Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina*."

Yesu – kwa sababu ni mwokozi wetu. Mat. 1:21, "*Naye atazaa mwana nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*"

Emanueli – Kwa sababu ni Mungu pamoja nasi. Mat. 1:23, "*Tazama bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli; naani Mungu pamoja nasi.*"

Bwana – kwa sababu ni mtawala. Mat. 3:3, "*Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya akisema, sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake.*"

Kristo – kwa sababu ni mpakwa mafuta wetu. Mat. 16:16, "*Simoni Petro akajibu akasema , Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.*"

Mariamu, dada yake Martha, alimpaka Yesu mafuta kichani na miguuni na akafuta miguu yake kwa nywele zake. Mitume walichukia kwa sababu alitumia mafuta yenye gharama kubwa. Yesu akasema katika Marko 14:8, "*Ametenda alivyoweza; ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko.*"

Adamu wote walioa.

Mungu alimtengenezea Adamu mwanamke.

Mwa. 2:18, 21-23, "*BWANA Mungu akassema si vyema mtu huyo akawa peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye…Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume.*"

Yesu alipewa mwanamke – kanisa.

2 Kor. 11:2, "*Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja; ili nimlete Kristo bikira safi.*"

Vitu kadhaa vilikuwa vinafanana katika mahusiano ya Adamu na Eva na Kristo na kanisa:

Mungu alisababisha usingizi mzito kuja kwa Adamu. Yesu alipaswa kulala usingizi wa mauti.

Rom. 7:4, "*Kadhalika ndugu zangu ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu kusudi tumzalie Mungu matunda.*"

Mungu alifunua ubavu wa Adamu; askari walichoma ubavu wa Kristo kwa mkuki.

Yoh. 19:34, "*Lakini askari mmoja wapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji.*"

Adamu alilipia gharama ya mwili wake na damu kwa ajili ya mwanamke. Kristo alilipa gharama ya damu yake kwa kanisa.

Mdo. 20:28, "*jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"

Hawa alikuwa mtoa msaada kwa Adamu; kanisa linasaidia kukutana na Yesu.

Adamu alikuwa na wake wangapi? Mmoja tu. Kristo anao wangapi?

Efe. 4:4, "*Mwili mmoja, na Roho Mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.*"

Mke wa Adamu wa kwanza alitumia jina lake. Aliitwa:

"**Mwanamke**" Mwa. 2:23, "*Adamu akasema sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume.*"

"**Adamu.**" Mwa. 5:2, "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.*"

"**Eva**" Mwa. 3:20, "*Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai.*"

Hivyo basi, alikuwa Hawa Adamu.

Tendo la mwanamke kutumia jina la mume wake lilianza na wanadamu wa kwanza.

Kanisa, bibi harusi wa Kristo, linapaswa kuvaa jina la Kristo.

- Rom. 16:16, "*Salimianeno kwa busu takatifu, makanisa ya Kristo yawasalimu.*"
- Mdo. 4:12, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Ulinganifu wa Adamu wawili

Adamu alitenda dhambi katika majaribu. Kristo aliepukana na dhambi ya majaribu katika maisha yake yote.

Dhambi ya Adamu iliathiri familia yote ya mwanadamu.

Rom. 5:12, "*Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi;*"

Kifo chake Kristo kiliathiri familia yote ya wanadamu.

1 Kor. 15:20-22, "*Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalikaa na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*"

Hitimisho

Kwa wale wanaokufa katika Kristo, nguvu ya kufa haiwezi kuingilia pumziko lao la milele.

Ufu. 14:13, "*Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate pumziko baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafutana nao.*"

Upumbavu wa Kuamini katika Hekima za Mwanadamu

na

Ellis P. Forsman

(The Folly of Trusting in Human Wisdom)